

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA NISHATI NA MADINI
CHUO CHA MADINI DODOMA
S. L. P 1696, Dodoma
Simu: +255 26 2300472, Fax: +255262963003
Barua pepe: info@mri.ac.tz/principal@mri.ac.tz/registrar@mri.ac.tz
Tovuti: www.mri.ac.tz



(Kimepewa Ithibati kamili na NACTE)

NAFASI ZA KUJIUNGA NA MASOMO KATIKA NGAZI YA ASTASHAHADA/STASHAHADA KWA MWAKA WA MASOMO 2017/2018

Chuo cha Madini Dodoma kipo chini ya Wizara ya Nishati na Madini, kina uzoefu wa zaidi ya miaka thelathini (30) katika kufundisha wataalamu wa ngazi ya kati katika sekta ya madini. Tangu mwaka 2012, Chuo cha Madini kilianza pia kutoa mafunzo katika sekta za Mafuta, Gesi na Mazingira.

Chuo kimepewa ithibati kamili na Baraza la Taifa la Mafunzo ya Ufundi (NACTE) kutoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada hadi Stashahada (NTA level 4 - 6) katika mfumo wa umahili (CBET) tangu tarehe 27/4/2007.

Chuo kinakaribisha maombi kwa waombaji wenye sifa kuomba kusoma Astashahada/Stashahada kwa kozi zifuatazo:

- **Jiolojia na Utafutaji Madini (Geology and Mineral Exploration)**
- **Uhandisi Migodi (Mining Engineering)**
- **Uhandisi Uchenjuaji Madini (Mineral Processing Engineering)**
- **Sayansi ya Mafuta na Gesi (Petroleum Geosciences)**
- **Uhandisi na Usimamizi wa Mazingira Migodini (Environmental Engineering and Management in Mines)**

Hakutakuwa na ufadhili kwa waombaji watakaochaguliwa katika kozi zote

SIFA ZA KUJIUNGA

- Mwombaji awe amemaliza kidato cha nne (Form IV) na awe amefaulu masomo ya Fizikia, Kemia, Hisabati na masomo mengine mawili (2) kwa kiwango cha kuanzia D; au
- Awe na cheti cha kuhitimu Elimu ya Sekondari pamoja na Cheti cha VETA ngazi ya ufundi sadifu katika fani za Uhandisi Umeme, Mitambo au Ujenzi.

NAMNA YA KUTUMA MAOMBI

Waombaji wote wenye sifa wanatakiwa wajaze fomu ya maombi na kuituma Chuoni moja kwa moja. Fomu za maombi zinapatikana Chuoni, Ofisi za Wizara ya Nishati na Madini, Ofisi za Madini zilizopo Mbeya, Tabora, Mwanza, Kahama, Dar es Salaam, Musoma, Songea, Arusha, Tanga, Tunduru, Dodoma, Morogoro, Handeni, Merelani, Mpanda, Bukoba, Mtwara, Shinyanga, Chunya, Moshi, Nachingwea, Geita, Bariadi, Singida na Kigoma, au katika tovuti ya chuo: www.mri.ac.tz

AU;

Unaweza kutuma maombi kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa NACTE; <http://www.nacte.go.tz/Central Admission System>.

Kwa maelezo/msaada zaidi wasiliana nasi kupitia: 0784 893 116 / 0764 910 385 / 0717 361 771 / 0753 858 028

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 31/5/ 2017 saa 9:30 alasiri.

Tarehe ya kuanza masomo kwa mwaka wa masomo 2017/2018 ni 21/8/2017.

NB:

- Kwa wale watakaotuma fomu za maombi yao Chuoni, waambatanishe na nakala halisi ya hati ya malipo ya benki (Pay-in Slip) yenye kiasi cha Tshs. 20,000/= na ilipwe kwenye akaunti ya Chuo (Akaunti Na. 01J1082316900, CRDB, CHUO CHA MADINI DODOMA).

Fomu za maombi zitumwe kwa:

Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Madini Dodoma,
S. L. P 1696,
Dodoma